# LEARNING BY EAR.

## Lent Luxury- The risks of raising credit.

## EPISODE EIGHT: THE CONSEQUENCES.

**AUTHOR: James Muhando**

**EDITORS: Adrian Kriesch, Friederike Müller**

**PROOFREADER: Tony Dunham**

**KISUAHELI: Eric Ponda**

**<u>LIST OF CHARACTERS BY SCENE:</u>**

**<u>SCENE ONE: AT JD'S.</u>**

- **LUKA(M 40'S)**
- **NINA(F 35)**
- **JD(M 15)**
- **NARRATOR (M 30)**

**<u>SCENE TWO: AT SCHOOL.</u>**

- **NARRATOR (M 30)**
- **MR.GEORGE MANDO (M 40)**

- **NAUGHTY STUDENT (F/M 15)**
- **WINNIE (F 15)**
- **4-6 CROWD OF LAUGHING STUDENTS (around 15 years-old)**

**SCENE THREE: AT JD'S.**

- **LUKA (40's)**
- **NINA (F 35)**

**SCENE FOUR: IN DUNGA TOWN.**

- **NARRATOR (M 30)**
- **CAR WASH MANAGER (M 30'S)**
- **JD (M 15)**

**SCENE FIVE:ON THE ROAD.**

- **GIDDY (M NOW 17)**
- **JENNY (F NOW 17)**
- **TOBBY (M NOW 18)**
- **JD (NOW 17)**
- **NARRATOR (M 30)**

**INTRO:**

1. **SFX: OFFICE AMBIENCE**
2. **NARRATOR:**

Hujambo na karibu katika sehemu ya nane katika mfululizo wa mchezo huu kuhusu "**Starehe za kuazima-Tatizo la kulipa Mkopo**"*.* Karibu ofisini mwangu japo ndogo katika benki hii ninapo fanya kazi kama afisa wa masuala ya Mikopo. Kukukumbusha tu, jina langu ni Gideon Leboo au Giddy. Mimi ndiye mhusika mkuu katika mfulululizo wa hadithi hii. Na bado nakusimulia kuhusu maisha ya ujana wangu, na jinsi nilivyouchezea. (Laughs). Katika kipindi kilichotangulia, Gori, ambaye kazi yake ni kukopesha pesa, anakamatwa na maafisa wa Polisi baada ya kumvunja mkono Jenny, akidai pesa zake. Pia mjombangu Barry ahukumiwa kifungo cha miaka miwili gerezani kwa kushindwa kulipa deni lake. Kwa upande mwengine rafiki yangu JD anajikuta mashakani kwa kuchukua baiskeli kwa mkopo na kushinda kulipa pesa hizo. Matatizo ya JD yanaongezeka baada ya babake

kurejea nyumbani kutoka safarini, na kufahamisha kuhusu masahibu yanayomkuta mwanawe.

**SCENE ONE: AT JD'S.**

3. **SFX:** **NIGHT SOUNDS.**

4. **SFX:** **KNOCK ON THE DOOR.**

5. **LUKA:** **(Drunk from outside)** Nifungulie mpenzi wangu Nina! Nifungulie mlango! Mumeo unayemchukia sasa amerudi nyumbani! Nifungulie!

6. **NINA:** **(Surprised)** Huyo ni Babako? Na ni mlevi nini? Babako hanywi pombe!

7. **JD:** Sidhani amelewa!

8. **NINA:** Nenda ukamfungulie mlango!

9. **SFX:** **FOOTSTEPS, DOOR OPENS.**

10. **LUKA:** **(To Nina)** Na wewe ni nani? Huyu jambazi anafanya nini hapa? Mimi nimesema sitaki kukuona tena hapa nyumbani kwangu?

11. **NINA:** Luka? Umelewa?

12. **LUKA:** Swali haliwezi kujibu swali! Nimekuuliza swali!

13. **NINA:** Luka, huyu si mtoto wako! Ni kweli amefanya makosa na anastahili kuadhibiwa!

14. **LUKA:** Makosa? Huyu kijana ameniaibisha sana mbele ya marafiki na kijiji kizima! Na sasa maadui zangu wanafurahia sana kuniona niko mashakani! Na eti ni kosa limetokea?

15. **NINA:** Luka, tuwache kulaumiana. Hebu tutafute pesa za kulipa hili deni ili kuikomboa redio iliyochukuliwa na JD na rafiki zake..

16. **LUKA:** **(Firmly)** Mtu mmoja tu ndiye kichwa cha nyumba hii. Nimesema JD aondoke au mimi niondoke! Sasa amua!

17. **SFX:** **FOOTSTEPS AS FATHER LEAVES**

18. **NINA:** Mume wangu....!, JD tafadhali!

19. **JD:** Ni sawa mama, nitaondoka.

20. **NINA:** Unaondoka? Kwenda wapi?

21. **JD:** Nina marafiki wengi sana. Pia naweza kwenda kuishi na bibi..

22. **NINA:** Huendi mahali popote! Nimeweka akiba ya pesa kigodo, kesho asubuhi nitakupa ukalipe deni ili uweze kurejeshewa redio.

**23. NARRATOR:**

Baada ya kufanya kazi kwa muda, sasa kama ofisa wa masuala ya mikopo, naweza kusema kuwa mambo haya ni dhahiri. Hapa barani Afrika ni kina mama ndio wenye busara na fikra ya kuweka akiba. Wanaume pia wanapaswa kuiga mfano huo wa kinamama! Hata hivyo lakini, wakati Gideon alipokuwa bado ni Giddy, pia alikuwa na ujinga huo huo! Afadhali yule ofisa wa usalama alikuwa akijua alichokuwa akikifanya!.. kutuadhibu kisha kutupa mafunzo kuondoa ujinga wetu.. Aliweza kumtumia mtaalam kutupa mafunzo kuhusu masuala ya mikopo na jinsi ya kujiepusha na mikopo isiyo na umuhimu wowote. Hata hivyo, lakini jambo hili halikuwafurahisha vijana wengine waliolichukulia kimzaha suala hili, eti kwa sababu ya kuteswa, na kulazimishwa kuketi kwa muda kwa saa nyingi.

**<u>SCENE TWO: AT SCHOOL</u>**

24. **SFX: CLASSROOM AMBIENCE.**

25. **MR. MANDO:** Habari ya mchana. Naitwa George Mando. Nafanya kazi katika benki ya Jubilee kama neneja msaidizi. Ofisa wa polisi na mwalimu wenu Bi. Mando ambaye pia ni mke wangu, wameniuliza kuja hapa kuwapa mafunzo kuhusu masuala ya mikopo na tatizo katika kulipa mikopo hiyo. Lakini kabla sijaanza ,nini mnachofahamu kuhusu mikopo? Nani anayejua?

26. **NAUGHTY STUDENT: (Naughtily and not so loud)** Maana ya Mkopo ni JD!

27. **STUDENTS: LAUGH.**

28. **MR.MANDO: (Not really meaning it)** Ha! Ha wachekesha! Nani mwengine ambaye hatalichukulia kimzaha suala hili? Ehhe, wewe? Unaitwa nani?

29. **WINNIE:** Jina langu ni Winnie.

30. **MR. MANDO:** Naam Winnie! Mikopo ni kumaanisha nini?

31. **WINNIE:** Maana ya mkopo ni kitendo cha kuazima..

32. **MR. MANDO:** Vyema kabisa! Mkopo ni pesa unazopewa kwa muda na hatimaye kuzilipa baadaye. Lakini kwani watu

wachukue mikopo? Watu huchukua mikopo kwasababu ya kutaka kushughulikia mahitaji yao ya dharura!

33. **NAUGHTY STUDENT: (In jest)** Kama kununua baiskeli!

34. **STUDENTS: LAUGH.**

*35.* **MR. MANDO: (Ignores them)** Wakati mtu anapochukua mkopo na kukosa kulipa katika muda uliokubaliwa, basi tunasema ameshindwa kulipa.

36. **NARRATOR:**

Kwa hivyo, akaendelea kuzungumzia nasi kuhusu masuala ya mikopo na tatizo la kushindwa kulipa madeni, ni jinsi mtu anavyoweza kuepukana na madeni. Kilikuwa kikao chenye mafunzo mengi sana. Lakini niliona kama kupoteza wakati kwasababu, mtu aliyehitaji kupewa mafunzo haya alikuwa JD ambaye hakuweko kwenye kikao siku hiyo: JD alikuwa wapi wakati huo? Ofisa wa polisi alikuwa ametuagiza mimi, Jenny na JD kufika kituo cha polisi ili kuhudhuria vikao hivyo. Lakini JD ametoweka baada ya mamake Nina kumpa dola 60 kwenda kulipa deni la redio tuliyoiba nyumbani kwetu. Lakini alikuwa hajamlipa mama pesa hizo! Na ni wiki moja sasa tangu JD aonekane. Mzozo ulikuwa umezuka nyumbani kwao!

***KW begin***

**SCENE THREE: AT JD'S.**

**37. LUKA:** **(Aggressive)** Nenda ukamlete mtoto wangu sasa hivi. Umemficha wapi?

**38. NINA:** Samahani. Sasa unanilaumu mimi Luka?

**39. LUKA:** **(Firm)** Nataka kumuona mtoto wangu!

**40. NINA:** **(Mimicking him) "**Mwambie sitaki kumuona nyumbani kwangu! Au si ni wewe uliyeyasema maneno haya? Na sasa kwa nini unanilaumu?

**41. LUKA:** Unadhani sina habari kwamba ulimpa pesa, ili kwenda mafichoni?

**42. NINA:** Kwanini unanilaumu kwamba nimemficha mtoto wako, wakati mimi na wewe tumekuwa tukizunguka kumtafuta kila mahali? Usijaribu kunilaumu Luka!

**43. LUKA:** Unasema nisikulaumu?. Unafikiri nafanya mzaha?Toka nje..!, pia wewe sitaki kukuona hadi pale utakaporejea nyumbani na JD!

**44. NINA:** Nitamtoa wapi sasa?

**45. LUKA:** Mimi sijui, wewe unajua ulikomficha!

**46. NINA:** Luka…

**47. LUKA:** Toka nje!

**48. NINA:** Sawa! Lakini usije kunitafuta!

**49. SFX: FOOTSTEPS, DOOR OPEN.BANGS SHUT!**

***KW END***

## SCENE FOUR: IN A NEIGHBOURING TOWN

**50. NARRATOR:**

Rafiki yangu mwema JD ametoroka kijijini baada ya kupewa pesa na mamake. Dola 60 zilikuwa pesa nyingi kwake na akadhani angeweza kuishi vizuri! Isitoshe babake hakutaka kumuona nyumbani huku akiwa na dhana kwamba marafiki wake wote pia wamemtenga. Alikuwa amesikia kwamba ni rahisi kuajiriwa mjini, hivyo akaamua kuelekea mjini. Lakini muda si muda, akaja kufahamu kwamba mambo hayakuwa rahisi jinsi alivyodhania. Ulitumia pesa zote Dola 60 alizopewa na mamake ndani ya muda wa wiki mbili tu, kugharamia malazi na matumizi mengine. Kazi yake ilikuwa ni kuosha

magari ambapo pesa alizolipwa zilimtosha tu kwa chakula cha mchana.

51. **ATMO: TOWN AMBIENCE.CAR WASH SOUNDS.**

52. **CAR WASH MANAGER:** **(Shouts in an unfriendly tone)** Wewe mshamba! Umeosha haya magari kama nilivyokuagiza?

53. **JD:** Ndio nimeyaosha.

54. **CAR WASH MANAGER:** Muongo wewe! Haya magari hayaonekani kama yameoshwa! Hebu tazama magurudumu. Yamejaa tope.

55. **JD:** Lakini nimeyaosha na kurudia karibu mara tatu. Kuna magari mengine kumi yananisubiri na tayari giza limeanza kuingia. Sasa nitamaliza saa ngapi?

56. **CAR WASH MANAGER:** Wewe mvivu!.., mshamba usiyejua lolote...! Rudi nyumbani huko Mashambani! Leo hakuna mshahara..sikulipi!

57. **JD:** **(Not so loudly)** Ni sawa! Kama ambaye wanilipa siku zote.!

58. **CAR WASH MANAGER:** Samahani? Umesema nini?

**59. JD:** Sijasema lolote. Samahani. Tafadhali usinifukuze kazini! Nitajibidisha!

**60. CAR WASH MANAGER:** Nyinyi vijana wa mashambani mnasahau haraka sana!.. Siku chache tu umekuja hapa na matambara ukiwa na njaa. Sasa nimekupa chakula ...waanza kuwa mjeuri?

**61. JD:** Samahani.

**62. CAR WASH MANAGER:** Rudi kazini uendelee na kazi yako! Lakini nitakupa nusu ya pesa zako za chakula cha mchana wa leo!

**63. JD:** Asante sana Mzee..

**64. SFX:** **HOSE PIPE SPRAYING WATER AS HE GETS BACK TO WORK**

**65. NARRATOR:**

Baada ya kazi, JD alikuwa akijifanya kwamba anaenda nyumbani kulala, lakini kumbe mahali hapo pa kuoshea magari ndio yaliyokuwa makaazi yake baada ya wengine wote kwenda nyumbani . Hakuwa na mahala pa kulala. . Licha ya mateso aliyopitia kwa muda wa wiki chache hivi, JD alishindwa kurudi nyumbani. Hakuwa na marafiki! Lakini alifahamu kwamba kila mmoja alikuwa ana wasi wasi kuhusu maisha yake! Tulijaribu

kumtafuta kila mahali! Na hata mamangu hakuwa ametaka kulipwa pesa za redio. Ni babake tu ambaye alisisitiza alipe! Baada ya miezi michache, Mimi na Jenny tukafanya mtihani wetu wa mwisho.

**SCENE FIVE: ON THE ROAD.**

**66. ATMO: COUNTRY AMBIENCE**

**67. SFX: FOOTSTEPS AS THEY WALK HOME.**

**68. GIDDY:** Mtihani wa hesabu ulikuwaje?

**69. JENNY:** Ulikuwa mgumu sana! Lakini natumai nitapita. Na wewe je?

**70. GIDDY:** Niliuona rahisi, hasa kufanya hesabu ya kutafuta kiwango cha riba!

**71. JENNY:** Lakini wewe ni hodari sana kwa masuala ya hesabu. Bado una azma ya kusomea sheria utakapojiunga na chuo kikuu?

**72. GIDDY:** Sitaki tena. Sasa nataka kufanya kazi katika benki. Nataka kufanya kazi kuhusu masuala fedha.

**73. SFX: COMMOTION FROM AFAR AS TWO PEOPLE FIGHT.**

74. **TOBBY:** **(Conversation between Tobby and JD: Off mike/from a distance)** Ulifikiri sitakushika! Nirudishie pesa zangu!

75. **JD:** **(Rudely)** Pesa gani?

76. **TOBBY:** Zile nilizokukopesha na kisha ukatoweka!

77. **JD:** Lakini kwanza nilihitajika kulipa mkopo wa baiskeli yangu uliyogonga!

78. **TOBBY:** Lakini uliniahidi kunilipa! Kama ningejua hutanilipa, kamwe nisingekukopesha!

79. **JD:** **(Defiant)** Basi sitakulipa pesa zako!

80. **TOBBY:** Una uhakika? **(Punches him)** Utazilipa pesa zangu. Lazima utazilipa!

81. **JD:** Nami nasema sitakulipa!

82. **JENNY:** **(close mike)** Na yule si JD JD?

83. **GIDDY:** Ndio. Amebadilika sana, nini kilichompata? Anaonekana mzee sasa!

84. **JENNY:** Kwani anazozana na Tobby! Fanya upesi! Twende tukawatenganishe!

85. **SFX:** **FOOTSTEPS AS THEY RUN TO SEPARATE THEM.**

86. **JENNY:** Wacheni kuzozana! JD!

87. **GIDDY:** Tobby, wacheni kupigana tafadhali!

**<u>OUTRO:</u>**

**89. SFX: OFFICE AMBIENCE.**

**90. NARRATOR:**

Baada ya ziara hii fupi ya miaka miwili tangu JD aondoke nyumbani tayari alikuwa amenza tabia ya kunywa pombe na kuvuta sigara. Alioneka mchafu na aliyedhoofika sana kiafya. Lakini aliporejea, bado masahibu yalikuwa yakimsubiri. Najua wengi wanatamani sana kukopa ili waweze kununua vitu vya thamani na vya kisasa kama vile simu za mkononi, au kamera za kisasa. Je! Wafikiri kisa hiki cha JD kina funzo lolote kwako? Na ndio sababu nikakubali kufanya kazi kama mshauri wa masuala ya mikopo katika benki hii ili niweze kutoa ushauri kwa vijana. Wakati vijana wengi wanapohisi kukabiliwa na matatizo ya kifedha, mara nyingi hufika ofisini kwa ushauri na baada ya kujadiliana tukapata suluhisho la ni jinsi gani wanavyoweza kuongeza kipato au akiba zao bila ya kuchukua mkopo. Sawa kabisa msikilizaji, hapo ndipo tunafika mwisho wa makala haya leo, nikitarajia kwamba utaungana nasi tena ili niweze kukueleza mengi kuhusu JD baada ya kurudi nyumbani. Hadi wakati mwengine, kwaheri kwasasa.